
Ocular Films | A Free Guide

Ocular films

JINSI YA KUJIFUNZA CHOCHOTE KWA HARAKA



Hatua 7 za kuwa mzuri kwenye skill yoyote, kuanzia content mpaka sales, haraka kuliko watu wanaokuzunguka.

FREE GUIDE NA

Med · @he.is.med

IMETOKANA NA

Alex Hormozi · Ep 1011

KWA AJILI YA

Wafanyabiashara na creators

Hatua ya 1: Elewa kujifunza ni nini



"Intelligence is speed of learning." Hujabaki nyuma kwa sababu huna akili. Umebaki nyuma kwa sababu unajifunza taratibu, na hilo linabadilika.

01

Kujifunza

Hali ile ile, tabia mpya. Kama bado una-react vile vile, bado hujajifunza.

02

Intelligence


Kasi yako ya kujifunza: majaribio machache kupata sahihi, au majaribio mengi kwa muda mfupi.

03

Skill

Mnyororo wa tabia ndogo ndogo ulizozirekebisha mpaka zinafanya kazi pamoja.

Hatua 7 kwenye page moja



Hatua ya 1 ni kuelewa kujifunza ni nini. Zilizobaki sita ziko kwenye stages tatu: jipange, wasome walio bora, halafu rudia kwa kasi.

JIPANGE	WASOME WALIO BORA	RUDIA KWA KASI
Jua hasa unajifunza nini	Jua nini kinafanya kazi	Igeuze kuwa skill
2. Igawanye kwenye subskills	**5. Waangalie walio juu**	**6. Fanya reps**
3. Eleza success ni nini	**5. Fuatilia feedback yako**	**7. Fupisha mzunguko**
4. Angalia vitendo, sio akili	**6. Tafuta tofauti**	**Acha neno 'bahati'**

Anayeimprove kwa kasi zaidi ndiye anayeshinda mwisho. Sio mwenye kipaji zaidi, wala aliyeanza vizuri.

Jipange: jua unajifunza nini

"Kuwa bora kwenye content" ni kubwa mno kujifunza. Ifanye ndogo, wazi na inayoonekana.

Hatua ya 2: Igawanye kwenye subskills

Skill kubwa ni skills nyingi ndogo. Jifunze moja moja.

JARIBU HII

"Kutengeneza Reels" inakuwa: hook, kurekodi, mwanga, editing, captions, call to action.

Hatua ya 3: Eleza success ni nini

Kama huwezi kuipima, huwezi kujua kama unaimprove.

JARIBU HII

Chagua namba moja kwa kila subskill. Kwa hooks: watu wangapi bado wanaangalia sekunde ya 3.

Hatua ya 4: Angalia vitendo, sio akili

Huwezi kuiga confidence au kipaji cha mtu. Unaweza kuiga anachokifanya.

JARIBU HII

Badala ya "yeye ni natural kwenye camera", andika: eye contact, sentensi fupi, anaanza katikati ya stori.

Wasome walio bora: jua nini kinafanya kazi



Usianze kubahatisha kutoka sifuri. Majibu tayari yako kwenye kazi za wanaoshinda.

Hatua ya 5: Waangalie walio juu

Soma 10% ya juu ya matokeo kwenye fani yako, sio ya kawaida.

JARIBU HII

Save video 10 zilizofanya vizuri zaidi kwenye niche yako, uchambue sekunde zao 3 za kwanza.

Hatua ya 5: Fuatilia feedback yako

Matokeo yako yanakwambia nini kinafanya kazi. Andika, usitegemee kumbukumbu.

JARIBU HII

Sheet simple: tarehe, ulichojaribu, namba, note moja.

Hatua ya 6: Tafuta tofauti

Weka kazi yako pembeni ya kazi bora. Hiyo gap ndio somo lako linalofuata.

JARIBU HII

Angalia video yako na ya juu moja baada ya nyingine. Orodhesha kila tofauti unayoiona.

Rudia kwa kasi: igeuze kuwa skill



Kujua sio kujifunza. Umejifunza pale tabia yako inapobadilika, na hiyo inahitaji reps.

Hatua ya 6: Fanya reps

Rekebisha tofauti moja kwa wakati, halafu rudia mpaka tabia mpya iwe automatic.

JARIBU HII

Andika hook ile ile kwa njia 10 tofauti kabla hujarekodi.

Hatua ya 7: Fupisha mzunguko

Anayejaribu, kupima na kurekebisha haraka zaidi ndiye anayesonga mbele. Kwa mtu na kwa biashara.

JARIBU HII

Toka video moja kwa wiki mpaka tatu. Feedback mara tatu, kujifunza mara tatu.


Acha neno 'bahati'

Bahati haielezi kitu unachoweza kurudia. Jikite kwenye unachoweza kuona, kupima na kurudia.

JARIBU HII

Post ikifeli au ikifanya vizuri, uliza "nimefanya nini tofauti?", sio "nilikuwa na bahati?"

Mzunguko wako wa kujifunza: maswali 6



Pitisha skill yoyote mpya kwenye maswali haya kila wiki. Kila jibu liwe kitu unachoweza kuona au kuhesabu.

1	Najifunza nini hasa? Subskill gani moja wiki hii?
2	Namba gani inaniambia kwamba ninaimprove?
3	Nani ni 10% ya juu kwenye hili, na wanafanya nini hasa?
4	Tofauti kubwa kati ya kazi yangu na yao ni ipi?
5	Nimefanya reps ngapi wiki hii, na nawezaje kufanya zaidi?
6	Nimebadilisha nini, na namba yangu imefanyaje?

Mambo ya kufanya, na mambo ya kuepuka

Fanya	Epuka
Jifunza subskill moja kwa wakati	Kujaribu ku-master skill nzima kwa mpigo
Pima maendeleo kwa namba moja wazi	Kuhukumu kwa unavyojisikia
Iga wanachofanya walio juu	Kuiga wanavyoonekana, au watu wa kawaida
Fanya reps nyingi, kwa kasi	Kusubiri mpaka ujisikie uko tayari
Uliza ulifanya nini tofauti	Kulaumu bahati, algorithm au kipaji

Mfahamu creator



Med

@he.is.med

Filmmaker, content creator & strategist
Certified Public Accountant (CPA) · AI Native

Now nimefanikisha ukuaji wa brands mbalimbali kupitia content, zikiwemo brands zangu mwenyewe. Kila kilichopo kwenye hii pdf ni vitu ninavyovifanyia kazi kila siku kwa wateja wangu na kwenye biashara zangu binafsi.

Hii guide ya bure ni favor yangu kwako. Sasa nitafurahi kama na wewe utanifanyia favor kwa ku-follow business pages zangu.

Ocular Films

Creative production company: commercials, UGC na social media content kwa biashara.

@ocular.films
ocularfilms.com

TimePoint Dar

Saa original kwa bei unayoiweza, tunakuletea popote Dar es Salaam.

@timepointdar
timepointdar.com

Lux Wedding Experience

Wedding films na picha zinazokufanya uikumbuke siku yako tena na tena.

@luxweddingexperience
luxweddingexperience.com

Unahitaji content ya biashara yako? DM @ocular.films au tembelea ocularfilms.com